



TAARIFA KWA UMMA

Benki Kuu inapenda kutoa ufafanuzi kwa umma kuhusu taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii zinazotokana na kushuka kwa riba ya dhamana za serikali.

Kushuka na kupanda kwa riba za dhamana za serikali kunategemea nguvu ya soko na siyo uamuzi wa Benki Kuu.

Dhamana za serikali, huuzwa kwa njia ya ushindani (mnada) ambapo kila mwekezaji anawasilisha zabuni inayoonyesha bei ambayo yuko tayari kulipa kulingana na mahitaji na uwezo wake. Benki Kuu kama wakala wa serikali, hushindanisha maombi ya wawekezaji kufuatana na kiasi ambacho serikali imepanga kukopa kwa mnada husika. Ushindani huu ndiyo unaotoa riba ya soko.

Kushuka kwa riba ya dhamana ni ishara ya kuwepo kwa ukwasi mwingi na hii inaendana na sera ya kujenga mazingira ya kuongeza mikopo kwa sekta binafsi.

Imetolewa na:

Idara ya Uhusiano na Itifaki
BENKI KUU YA TANZANIA
botcommunications@bot.go.tz

22 Februari, 2018